

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



22 JUNI, 2021



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI NA SITA – TAREHE 22 JUNI, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**465. MHESHIMIWA DEUS CLEMENT SANGU (KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga katika Mji wa Laela baada ya agizo la Serikali la kuhamisha Makao Makuu.

**466. MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurasimisha Vitambulisho vya Wajasiriamali wadogo.

### **OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

#### **467. MHESHIMIWA LATIFA KHAMIS JUAKALI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Mashindano ya Michezo mbalimbali kila Mwaka wakati wa Sherehe za Muungano ili kudumisha hamasa za Muungano kwa Vijana.

### **WIZARA YA KILIMO:**

#### **468. MHESHIMIWA RIDHIWANI JAKAYA KIKWETE (CHALINZE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha maji ya Bonde la Ruvu yanatumika kwa Kilimo cha Umwagiliaji ili kukabiliana na changamoto ya usalama wa chakula.

**469. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE (LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni upi mpango wa Serikali katika kukwamua Zao la Chai nchini ambalo ni mionganini mwa Mazao ya kimkakati yenye changamoto nyingi.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**470. MHESHIMIWA DKT. JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini ujenzi wa Barabara ya Kyetema – Katoro – Kyaka utaanza na kukamilika kwa kiwango cha lami kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-2025.

**471. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara ya Njombe – Ndandu – Iyayi kuelekea Mkoani Mbeya.

**472. MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ujenzi wa barabara ya Tabora – Mbambali – Bukene – Itobo hadi Kahama umefikia hatua gani baada ya kutengewa fedha kwenye Bajeti ya Mwaka 2020/2021.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**473. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, nini kauli ya Serikali juu ya baadhi ya Askari wa TANAPA wanaolinda Hifadhi ya Msitu wa Marang inayopakana na Kata ya Buger Wilayani Karatu kujichukulia Sheria mkononi na kuua Wananchi wanaoingia kwenye Hifadhi.

## **WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

### **474. MHESHIMIWA JACKSON GEDION KISWAGA (KALENGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Serikali haioni uamuzi wa kutaka ifikapo Tarehe 01 Mei, 2021 Wasajili wa namba za Simu za mkononi mitaani (*freelancers*) wawe katika Maduka, unaweza kufuta ajira zaidi ya 40,000 na kudhoofisha lengo la ajira Milioni 8 ifikapo Mwaka 2025.

### **III. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali Kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Kwamba, Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**(Majadiliano yanaendelea)**


#### **IV. MUSWADA WA SHERIA YA SERIKALI:**

**(Kusomwa kwa Hatua zake zote)**

Muswada wa Sheria ya kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2021 (*The Appropriation Bill, 2021*).

**DODOMA  
22 JUNI, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**



**BUNGE LA TANZANIA**